# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**<u>STRATHMORE HIGH SCHOOL</u>**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# STRATHMORE SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**

**KARATASI YA 3**

**FASIHI**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**1. HADITHI FUPI - Damu nyeusi na Hadithi nyingine**

(a) Maneno haya ni ya mwandishi anamrejelea Fikirini. Ni baada ya Fikirini kupata kisanga cha kudanganywa na kuibiwa na Fiona kisha kuachiliwa na kuonywa asirudi huko tona. Baadaye anarudishiwa vitu vyake na kwenda chuoni.

(b) Mwanafunzi arejelee shida zote alizopata fikirini alipoenda ulaya kusomea huko. Baadhi ya majibu ni:

- Mhadhiri mzungu na wanafunzi darasani walikuwa wanamsaili maswali ya kumdhalilisha
- Alitozwa faini na polisi mzungu kwa kuvuka barabara huku taa za kuelekeza magari zimewaka rangi nyekundu
- Wahadhiri walitoa alama kwa kupendelea watu weupe na kukandamiza watu weusi
- Mama mzungu anapigia polisi simu anapoona hajafunga zipu ya suruali
- Dereva mzungu anapomwona Fikirini alijipurukusha kana kwamba hamna kituo rasmi pale na kumwacha.
- Fiona anamdanganya na kumpeleka Fikirini nyumbani kwake
- Fiona anamtaka Fikirini wafanye ngono naye
- Anamfungia kwa nyumba na kumwitia Bob anapoghairi kufanya mapenzi
- Anaamrishwa kuvua nguo zote
- Anatishiwa kuuliwa kwa kisu na pia anaelekezwa mtutu wa bunduki
- Ananyang'anywa pesa zote na stakabadhi zake ingawa zilirejeshwa baadaye

  Zozote tano 5 x 2 = 10

  (Taz: mwanafunzi anaweza rejelea kisa cha Fikirini na Fiona au matatizo yote yaliyomkumba)

(c) Sifa za Fikirini

-Ni mwenye bidii - Anajibidiisha kutafuta elimu ya juu marekani licha ya changamoto ambazo zinamkabili katika chuo kikuu. Anapoachwa na gari anaamua kwenda chuoni kwa miguu.

-Ni mvumilivu - Anapotukanwa, kudhalilishwa na kudunishwa na wanafunzi na wahadhiri wazungu anayavumilia matusi na kuendelea na elimu.
-Ni mwadilifu - Anakataa kufanya mapenzi na Fiona licha ya kutishiwa
-Ni mtiifu - Anatii yote anayoamrishwa na Bob na Fiona
-Ni mwenye kushawishika haraka. Anashawishika haraka kuundamana na Fiona (3 x 2) Mwalimu akubali hoja nyingine ya ukweli

**2. RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA**

(a) Muktadha
Haya ni maneno ya mashaka akijizungumzia mwenyewe baada ya kukutana na matuko weye anapokuwa akienda msalani kuisoma barua aliyopewa na Ben Bella katika uwanja wa Uhuru. (alama 4)

(b) Umuhimu wa Mashaka

- Ametumika kutahadharisha watu kuhusu kuwacheka vilema
- Ametumika kuonyesha umuhimu wa masomo/elimu kwa wanafunzi na umuhimu wa kutia bidii
- Ametumika vile vile kuwatahadharisha vijana dhidi ya kujiingiza katika mapenzi kabla ya ndoa.
- Ametumika kuonyesha, kuifichua hali ya kutowajibika kwa mwalimu majisufu ambaye hahudhuni vipindi shuleni
- Anaonyesha umuhimu wa kuwapa vijana uhuru.

(c) Umuhimu wa anayerejelewa
Anayerejelewa ni matuko weye

- Ametumika kufafanua/kueleza umuhimu wa uongozi bora
- Anaonyesha athari za umaskini katika Jamii
- Anaonyesha jinsi viongozi wanavyotepetea kazini kwani anadhalilishwa na kukosa kushughulikiwa
- Anaufichua uozo katika uongozi na kuonyesha kuwa viongozi wanaendeleza ukoloni mamboleo
- Ni kielelezo cha utetezi wa wananchi
- Anaonyesha umuhimu wa ucheshi
- Ametumika kuwazindua wananchi kuhusiana na haki zao
- Ametumika kueleza maswala ya ukoloni

- Mkongwe na dhuluma za wakoloni

(d) Mbinu za lugha

- Uzungumzi nafsia

- Maswali ya balagha

3. Ukiukaji wa haki za kibinadamu
    1. Ajira kwa watoto (Mf: DJ)
    2. Amani kudhulumiwa na Mtemi Nasaba Bora
    3. Mshahara duni mf Amani na Imani
    4. Ukosefu wa Elimu mf. D.J. Imani
    5. Mateso (Imani na Amani kwenye seli pia matuko weye
    6. Kupokonywa mali (familia ya Imani)
    7. Kupuuzwa kwa chweche makweche baada ya kuumia
    8. Mauaji (enzi za ukoloni)
    9. Haki ya mapenzi (Bi. Zuhara)
    10. Kupuuzwa kwa wagonjwa kwenye zahanati unaosababisha vifo (uhuru)

3b.

- Mwandishi anarejelea kisa cha Majununi alivyojenga nyumba mara tatu baada ya vita vya Dunia. Baadaye ilichukuliwa na mtemi Nasaba Bora. Kisa hiki kinaonyesha ujinga wa Major Noon.

- Imani alikumbuka alivyokutana na Amani mara ya kwanza karibu na ziwa Mawewa. Umuhimu wa kisa hiki ni kuwa Imani hakujiua.

- Baada ya Amani kukiokota kitoto, anarejelea kisa cha Fao. Kisa hiki kinaonyesha uvunjivu wa maadili katika Jamii

- Mtemi Nasaba Bora anapompata Amani chumbani na mkewe, anakumbuka jinsi mkewe alimpungia Amani mkono walipompita wakitoka kwenye sherehe za uhuru, jinsi alivyomtetea akiwa seli na hata anavyomtetea nyumbani. Umuhimu ni kumulika kinaya kilichopo

- Kisa cha familia ya Imani ilivyodhulumiwa kimetolewa kwa njia ya urejeshi

- Kisa cha msichana mlemavu mrembo aliyokuwa kwenye matwana na Nasaba Bora kimerejelewa wakati wa usimulizi

- Kisa cha DJ kufungwa katika jela ya watoto na alivyotoroka kimerejelewa kwa njia hii

- Kisa kilichopelekea maji ya kiberenge kutonywewa kimeelezwa kwa njia hii
  *Tanbihi: Mtahini lazima ataje wakati na mahali pa tukio katika kila jibu. Hoja hizi ni mwongozo tu. Mwalimu akubali hoja zingine za kweli Zozote 5 x 2 = 10*

a) Maneno haya ni ya Medi (√1) , akiwaeleza Meya, Tatu (√1) na Beka… walipokuwa ofisini (√1) mwa Meya. Walikuwa wameenda (√1) kumweleza Meya matatizo wafanyakazi wanayoyapitia. (4 x 1)

b)

1. Mishahara duni

2. Vitisho (watafutwa kazi)
   Mazingira duni (wanaosha vyuo bila glavu na ukosefu wa maji

3. Wananyimwa uhuru wa kujieleza (wanapoandamana wanatawanywa na askari

4. Wanadanganywa kuwa dawa zitafika (Daktari siki na waridi)

5. Viongozi hawayasikilizi malalamishi yao (Meya anadai hakuna pesa)

6. Kutolipwa mishahara kwa wakati unaofaa

7. Kukosa kuhusishwa katika vikao vya maamuzi (wawakilishi hawahusishwi na pia Diwani III

c)

1. Jasiri - anamwambia Meya wao wanapata mishahara mikubwa huku wafanyikazi wakiumia

2. Mwajibikaji - Anataka kuona matakwa ya wafanyikazi yameshughulikiwa

3. Mwenye msimamo dhabiti - Halegezi kamba hadi aone maslahi ya wafanyikazi yameshughulikiwa

4. Ni mjanja - Anapanga mgomo unaofaa

5a.

| **Mstahiki Meya** | **Diwani III** |
|---|---|
| Yeye ni <u>katili</u> - Anaidhinisha nyongeza ya mishahara kwa madiwani pekee | Mwenye <u>utu</u> - Anawajali wanacheneo |
| <u>Mwoga</u> - Anaogopa anapoelezwa kuwa mgomo ungekuwepo | <u>Jasiri</u> - Anamweleza Meya ukweli kuwa wafanyakazi ni muhimu |
| <u>Fisadi</u> - Anashirikiana na Bili kulifisidi baraza | <u>Mwadalifu</u> - Hashirikiani na madiwani wengine katika njama za kifisadi |

| | |
|---|---|
| Mwenye tamaa - Anatumia mali ya baraza la mji kwa manufaa yake | Mtetezi - Anatetea haki za wanacheneo kwa kumshauri Meya kuwaongeza mshahara |
| Msaliti - Amepewa uwezo wa kuwa kiongozi lakini hawashughulikii, anatumia nafasi hiyo kujinufaisha | Mwaminifu - Ni mwaminifu kwa wananchi waliomchagua. Anatoa ushauri unaofaa kwa Meya |
| Mwenye mtazamo finyu. Anakosa kuzingatia mpango wa kimaendeleo wa miaka kumi unaofaidi cheneo | Mshauri mwema- Anaonya kamati ya baraza dhidi ya kufanya maamuzi yenye madhara makubwa kwa baraza |

5.b.

- Waridi anasema kuwa, "Haraka haraka haina baraka' Kuhusiana na kuwasili kwa dawa. Anapendekeza kwamba wagonjwa wawe na subira kulikuwa na tetesi kuwa dawa zilikuwa karibu kuwasili

- Dkt. Siki anamwomba Waridi kuwapa wagonjwa tumaini kwani, ganga ganga za mganga huleta tumaini

- Meya anamwambia Bili kuwa, "mazoea yana taabu" uk 26. Hii ni kuhusiana na jinsi walivyozoea kukutana na kushirikiana katika mambo mengi

- Bili anamwambia Meya kuwa, mtumwa hauawi. Hii ni kuhusu uamuzi wa Meya kumlipa mwanakandarasi kwa niaba ya baraza

- Bili anamwambia Meya kuwa kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji kuhusiana na kelele za wafanyikazi wanaoandamana

- Diwani III anaambiana na Siki kuwa lililoandikwa halifutiki kuhusu kukutana kwao siku hiyo. Mkutano wao haukuwa na budi kufanyika

- Diwani III anamwambia Siki kuwa sikio la kufa halisikii dawa kwani Diwani anamshauri Meya lakini Meya anampuuza. Hali inapokuwa mbaya anajuta kwa kutomsikiliza diwani huyu

- Daktari Siki anamwambia Tatu kuwa watahadhari na mgomo wao kwani ni 'heri nusu shari kuliko shari kamili. Siki anajua kuwa migomo inaweza kuwa na madhara makubwa kwa baraza juu ya matatizo yaliyoko tayari

6. (a) Dagaa au Kijana (1 x 2)
   (b) Kuna urari wa vina

   - Lina beti tano

   - Mishororo mitatu katika kila ubeti

   - Lina pande tatu katika kila mshororo (4 x 1)

   (c) Matumizi ya lahaja mf. Magego – Meno

Inkisari – h'ondoa – huondoa
Kuburoga sarufi – Na wake udogo – Na udogo wake (3 x 1)

(d) Ukara – Vina vya utao na mwandamizi havitiririki, vya ukwapi vinatiririka.
Ukawafi – Pande tatu
Tathlitha – Mishororo tatu katika kila ubeti (3 x 1)

(e) Kijana nakupa mawaidha ya kwamba aliye cheoni kuhusishwa na makosa yote, kwa hivyo tia bidii afanyavyo mbogo uache kukaa. Chimbua mihogo utafute riziki (al. 4)

(f) Istiari / jazanda mf Jikaze kimbogo
Methali – mf ukubwa jaa
Msemo mf shika taa (kuwa mwangaza) (2 x 1) taja na kutoa mfano

(g) Toni ya matumaini
Toni ya kuhimizi
Toni ya kuonya (2 x 1)

**USHAIRI**

7

a. - Ni shairi huru kwa sababu mshairi ametumia (i) mishata mf. katu, eti, niondoke
- Shairi lina umbo la paa la nyumba
- Matumizi ya alama za uakifishaji kwa wingi (al. 2)

b. (i) Anatishwa kwa risasi
(ii) Kupigwa mateke na mikuki
(iii) Kuponda mali yake
(iv) Kuletewa hatimiliki bandia *(mwalimu akubali hoja nyingine yoyote)* Al. 4

c. (i) Huzuni
(ii) Ujasiri (2 x 1)

d. Shairi lina beti saba
Kila ubeti una mishororo sita
Lina umbo la paa la nyumba (3 x 1)

e. Usambamba – Ni urudiaji wa kiwango cha sentensi, kirai (n.k)
mf. (i) Niondoke, mimi niondoke hapa, niondoke hapa kwangu
(ii) Siondoki, siondoki, siondoki niondoke hapa kwangu (2 x 1)

f. Mshairi anasema kamwe hatoki kwake. Anaashiria chini ya mti waliozikwa babu zake na kusisitiza kwamba hawezi akaondoka (al. 3)

g. Inkisari – (i) Sendi – Siendi (ii) Nende wapi – Niende wapi (iii) Kuboroga sarufi mf yangu mimi ni ardhi hii – Ardhi hii ni yangu mimi (1 x 1)

h. Karatasi – Hati miliki
Nimesaki – Nimebaki
Kitovu – Asili (al. 3 x 1)

8. a. Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee (al. 2)

b. Sifa za mlumbi

1. Hutumia lugha kwa njia inayovutia na kushawishi hadhira
2. Mulumbi huwa jasiri (huhitaji kuwa mkakamavu)
3. Hutumia chuku kwa ufanifu mkubwa
4. Anapaswa kutumia vipengele anwani vya lugha kama shairi, methali, nahau, taswira nk.
5. Hutumia lugha kutegemea muktadha na hadhira yake
6. Huwa na kipawa cha kuwa viongozi katika Jamii (4 x 2)

c. Umuhimu wa Ngomezi
- Ni njia ya kupitisha ujumbe wa dharura katika Jamii mf. vita
-Ni kitambulisho cha Jamii
-Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Jamii
-Hukuza uzalendo (wanajamii huionea fahari mbinu hii ya kuwasiliana

-Hukuza ubunifu (jinsi wanajamii wanavyokabiliwa na aina tofauti tofauti za ujumbe ndivyo wanavyojifunza mitindo mipya

- njia rahisi ya kuwasilisha ujumbe (4 x 2)

d. (i) Toni katika runun u
   (ii) Kamsa/milio kwenye magari mf. ambulensi
   (iii) Kengele (2 x 1)